

# CHANGAMOTO TUNAZOKUTANA NAZO NDIZO

## ZIMEBEBA BARAKA ZETU.

MAANDIKO: ISAY. 41: 8 – 13, LUK. 22: 42 – 43

### 1. UTANGULIZI:

Katika Biblia, watu karibu wote maarufu na waliofanikiwa sana baadae, walifanikiwa katika changamoto zilizojitokeza katika maisha yao. **Na kwa kweli kabisa kiroho, changamoto ndiyo ngazi ya ushindi, mafanikio pamoja na baraka za Watakatifu.**

- Nimejifunza jambo moja kubwa kwamba Mungu daima **hamuondolei** mtoto wake changamoto ambazo anafahamu kwamba zimebeba hatima yake ya baadae (Baraka zake za baadaye); lakini yeye anafanya mambo makubwa **matatu** wakati mtoto wake anapokuwa anapitia katika changamoto nzito katika maisha yake:-

a. **Anamtia nguvu. Luk. 22: 42- 44 (1Wafal. 19: 4 – 21), Isay. 41: 10** (anakuwa upande wake kwa asilimia 100, **Rum. 8:31.**

b. **Anamsaidia:- Mwz. 19: 9-11, (Eliezeri), Kut. 18: 4, Zab. 20: 2, 46: 1, 60:11-12, 94: 17, Zab.121: 1- 2, n.k.**

c. **Anamshika mkono:- Math. 14:30-33,** (zipo changamoto ambazo bila kushikwa mkono na Bwana Yesu huwezi kutoka – **Dan. 3: 15 - 25, 6: 16 - 24.**

Lengo la Mungu la kufanya haya mambo makubwa (3) kwa watoto wake ni ili waweze kustahimili changamoto wanazopitia; na wakati huo huo yeye akifanya mambo makubwa ya baraka na mafanikio kwa mtoto wake ili apate kutukuzwa kupitia changamoto zetu.

### **2. Mambo matatu muhimu sana ya kufanya wakati wa changamoto tele katika maisha yetu.**

- a. Mwombe daima Mungu akutie nguvu wakati wa changamoto zako ili uweze kuvuka salama kama Yesu alivyoomba; yaani tumwombe Mungu ili atupe uwezo na sisi wa **kuhimili dhoruba, vikwazo, shida mateso** n.k. tunayokutana nayo baada ya kuokoka ili nasi baadae tuweze kuzifikia baraka zetu. **Luk. 22: 40 – 43.**

b. Siyo ndugu zangu kila mlima tunaokutana nao katika maisha haya ni wa kuamuru ung'oke na kutupwa baharini!!  
**Mark. 11: 23.** Milima mingine ni ya kupanda hadi kileleni ili upate mazoezi na uzoefu wa kiroho ili baadae uwe msaada kwa wengine. **Ayub. 42: 7-10, Filip.2:9 -11, Mwz. 45: 1 - 12.**

**Note:** Hakuna mlima usiokuwa na kilele, na ukifika kileleni mwa mlima tarajia kuanza kuteremka tu.

**Ayub.42:10-17, Mwz. 41: 37-45. Est. 8: 15- 17 n.k.**

c. Elewa kwa kina kwamba Mungu hatangulii kutubariki maadamu eti tumeokoka; anatangulia kutuwekea baraka zetu katikati ya changamoto ili tunapozishinda changamoto hizo ndipo tupokee baraka zetu.

**“Unajua:** Kila changamoto tunazokutana nazo (jaribu) mbele za Mungu zina utatuzi wake. Na kila changamoto (jaribu) aliyo nayo mteule Mungu anafahamu fika kwamba tunao uwezo wa kuishinda – **1Kor. 10: 13** yaani Mungu ametuamini kabisa na ametupatia uwezo wa kuzishinda changamoto hizo; na kwa hakika kiwango chetu cha kumjua Mungu kikiwa juu/kikiongezeka, ndipo kula mema ya nchi nako kunakuwa rahisi!!! **Ayub. 22:21.**

3. Sikia Mfalme Daudi aliyepitia changamoto nyingi kabla ya kutawala (**miaka 13**) ya misukosuko mingi anavyosema **“Zab. 119: 67, 71!! Ilikuwa ni vema kwamba ulinitesa kwanza.**

- Kila mahala ndugu zangu changamoto zipo tu tele, hata kama mtu angeamua kwenda kuishi porini peke yake ili aepuke makwazo, bado atakutana na ndege watakao mkojolea kichwani.

- Kupimwa na Mungu kabla ya kutupandisha daraja ni jambo la lazima kwa kila mteule. **Yusufu alipimwa, Mordekai pia, Danieli na wenzake walipimwa, Musa alipimwa, Daudi alipimwa, Ayubu zaidi sana!!!**

**Somo lijalo nitawafundisha juu ya aina tatu kuu 3 za majaribu.**

**Na**

**Askofu Dr. L. M. Mwizarubi**

**28/02/2021**

